


Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 05 Issue: 01 | March-2026

EAJK

# Tamthilia za Kiswahili kama Chombo cha Uhamasishaji kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu: Mifano ya *Mwinyi na Manyani ya Adili* na *Kodi*

**Author**
**Ogonda Samuel Sinzore**
**Author's email:** sasio.ogonda@gmail.com

**Kibabii University, Kenya.**

**Cite this article in APA**
Ogonda, S. S. (2026). Tamthilia za Kiswahili kama chombo cha uhamasishaji kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu: Mifano ya *Mwinyi na Manyani ya Adili* na *Kodi*. *Eastern Africa journal of Kiswahili, 5*(1), 32-41. https://doi.org/10.51317/eajk.v5i1.973

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 2026-01-21
Accepted: 2026-02-13
Published: 2026-03-17

Scan this QR to read the paper online

**Copyright:** ©2026 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

**Ikisiri**

Azma ya makala hii ni kuchunguza tamthilia za Kiswahili kama chombo cha kuhamasisha jamii kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME). MME ni mpango ulioidhinishwa na Umoja wa Mataifa mwaka 2015 na umekumbatiwa na serikali, mashirika na wasomi mbalimbali duniani. Utafiti huu ni wa kithamano na unaongozwa na Nadharia ya Uhistoria Mpya iliyoasisiwa na Stephen Greenblatt (1980) na kuendelezwa na Brizee na Tompkins (2012). Muundo wa kiuchambuzi ulitumika kuchunguza jinsi tamthilia teule zinavyoakisi na kuhoji masuala ya kijamii yanayohusiana na MME. Data ilikusanywa kwa mbinu ya unukuzi wa madondoo mahususi kutoka katika tamthilia teule kwa kutumia usampulishaji wa kimaksudi.Tamthilia zilizochaguliwa ni *Mwinyi na Manyani ya Adili* (Mbogo, 2022) na *Kodi* (Muhando, 2024) kwa sababu zinaangazia masuala ya MME na ziliandikwa kati ya mwaka 2016 na 2026, yaani kipindi cha utekelezaji wa malengo hayo. Matokeo yamewasilishwa kwa njia ya maelezo ya maandishi. Utafiti umebaini kuwa tamthilia hizi zinahamasisha kwa kiasi kikubwa malengo yafuatayo: L1 (kutokomeza umaskini), L2 (kutokomeza njaa), L5 (usawa wa kijinsia), L8 (ajira na ukuaji wa uchumi), L11 (miji na makazi endelevu) na L16 (amani, haki na taasisi imara). Masuala haya yanajitokeza kupitia wahusika, migogoro na maamuzi yao. Hata hivyo, malengo mengine kama L3 (afya bora), L4 (elimu bora), L6 (maji safi na usafi wa mazingira), L7, L9, L10, L12, L13, L14 na L15 hayajaangaziwa vya kutosha au yamepuuzwa kabisa. Makala hii inapendekeza kwamba waandishi wa tamthilia za Kiswahili wanapaswa kupanua wigo wa maudhui yao kwa kujumuisha kimaksudi malengo yaliyopuuzwa, hasa L3, L4 na L6, ili kuimarisha mchango wa fasihi katika uhamasishaji mpana wa MME.

**Maneno muhimu:** Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME), tamthilia, uchambuzi wa kifasihi, uhamasishaji, uhistoria mpya.

## UTANGULIZI

Fasihi ni muhimu katika kuhamasisha jamii kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME) (Mensah, 2019). Ingawa tafiti zilizopo zinaonyesha mchango wa fasihi katika maendeleo endelevu, nyingi zimejikita katika kazi za kifasihi za kimagharibi huku mchango wa tamthilia za Kiswahili katika kuhamasisha MME ukipuuzwa au kutochunguzwa kwa kina. Makala hii inalenga kuchunguza tamthilia za Kiswahili kama chombo cha uhamasishaji wa MME. Mpango huu unalenga kufikia maendeleo ya kijamii, usawa wa kijinsia, uhifadhi wa mazingira na ukuaji wa kiuchumi (UN, 2022). MME ni ajenda ya kimataifa yenye malengo 17, shabaha 169 na viashiria 232. Malengo na shabaha hizi zina uhusiano wa kukamilishana (Magendane & Kapazoglou, 2021).

Mazza (2021) anashadidia kuwa MME limekuwa eneo la kuangazia si tu katika uwanja wa kitaaluma bali pia katika mipango ya maendeleo ya mataifa mbalimbali. Kulingana na Mensah (2019), MME yamevutia umakini mkubwa kutoka kwa wasomi, viongozi na waratibu wa mipango. Mashirika mbalimbali ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali yamekumbatia MME kama dhana muhimu ya kimaendeleo. Katika utekelezaji wake, shirika la Umoja wa Mataifa kupitia Lengo la 17 linasisitiza umuhimu wa ushirikiano katika kufikia MME (Browne & Millington, 2015). Ushirikiano huu unahusisha taaluma mbalimbali. Tafiti mbalimbali zimebainisha kuwa fasihi inaweza kuchangia maendeleo na kuendeleza uafikiaji wa MME (Sterling, 2010; Edler & Park, 2021).

Tamthilia ni mojawapo ya tanzu za fasihi. Kulingana na Mlama (1991), tamthilia hujitokeza kupitia mazungumzo ya moja kwa moja na matendo ya wahusika. Tamthilia ina uwezo wa kuonyesha uhalisia wa jamii kwa njia ya moja kwa moja na ya kugusa hisia za hadhira au wasomaji. Hii inatokana na ukweli kwamba hoja katika tamthilia huwasilishwa kupitia migogoro, mivutano na maingiliano ya wahusika (Mazrui & Mazrui, 1995). Tamthilia ina uwezo wa kipekee wa kuwasilisha masuala ya kijamii kama uongozi, maadili, dhuluma, ukandamizaji na maendeleo ya jamii kwa njia ya wazi na yenye mvuto (Mazrui & Mazrui, 1995). Makala hii inashughulikia jinsi waandishi Emmanuel Mbogo na Penina Muhando walivyoliangazia suala la MME katika kazi zao ili kuhamasisha wasomaji na jamii kwa ujumla. Makala hii inajumuisha sehemu ya utangulizi, mapitio ya maandishi, mbinu za utafiti, matokeo, hitimisho na mapendekezo.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Sehemu hii inahakiki maandishi kwa kurejelea tafiti mbalimbali kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME). Musindalo (2020) alitafiti taswira ya haki za watoto katika riwaya za milenia mpya. Baadhi ya haki alizozichambua zinaingiliana kwa kiasi fulani na malengo ya MME. Hata hivyo, utafiti wake ulijikita katika riwaya na hauukuchunguza MME katika tamthilia.

Aidha, Sterling (2010) anasisitiza kuwa fasihi na elimu vina uwezo wa kubadilisha namna watu wanavyoiona dunia kwa kuchochea tafakuri ya kina kuhusu changamoto za kijamii na maendeleo. Kwa mtazamo huo, fasihi huwasaidia wasomaji au watazamaji kuelewa changamoto za maendeleo kwa mtazamo wa kibinadamu zaidi. Hata hivyo, utafiti wa Sterling haukujikita katika tamthilia za Kiswahili.

Vilevile, Edler na Park (2021) walichunguza nafasi ya utamaduni katika kufanikisha MME. Walibainisha kuwa utamaduni, ukiwemo fasihi, ni nyenzo muhimu katika kuhamasisha mabadiliko ya kijamii na kukuza maadili yanayounga mkono maendeleo endelevu. Utafiti wao ulikuwa wa kijumla, tofauti na kazi hii ambayo inalenga tamthilia mahususi za Kiswahili.

Isitoshe, tafiti mbalimbali zimeangazia matumizi ya fasihi ya kubuni kama nyenzo ya kufundishia MME. Kwa mujibu wa UNESCO (2017), fasihi inaweza kusaidia wanafunzi kuelewa masuala kama usawa, haki na uwajibikaji kupitia wahusika na matukio. Hata hivyo, utafiti wao ulijikita katika fasihi ya kimagharibi. Tofauti

na wao, makala hii inachunguza tamthilia za Kiswahili kama chombo cha kuhamasisha MME.

Ripoti za Umoja wa Mataifa (UN, 2022, 2023, 2024) zinaeleza kuwa utekelezaji wa MME unategemea sana uhamasishaji wa jamii kupitia elimu na vyombo vya mawasiliano vinavyoweza kubadilisha mitazamo ya watu. Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO, 2024) linasisitiza kuwa elimu ya MME inapaswa kuhusisha sanaa na utamaduni ili kuimarisha uelewa wa masuala ya kijamii, kiuchumi na kimazingira. Katika muktadha huu, fasihi ina nafasi muhimu kama chombo cha kuibua mijadala ya kijamii na kuhamasisha mabadiliko ya kitabia yanayohusiana na MME.

Kulingana UNESCO (2017), elimu ya ubora (L4) ni msingi wa kufanikisha malengo mengine ya MME. Kwa mujibu wa shirika hili, L4 inawawezesha wanafunzi na jamii kuelewa changamoto za maendeleo na namna ya kuzitatua. Hivyo, maandishi ya kifasihi yanaweza kuwa nyenzo muhimu ya kielimu katika kuhamasisha MME. Aidha, Bebbington et al. (2022) wanaeleza kuwa uendelevu unahitaji uwajibikaji wa kijamii na kiuchumi ambao unaweza kuhamasishwa kupitia mifumo ya maarifa, ikiwemo sanaa na fasihi.Kwa ujumla, tafiti hizi zinaafikiana kuwa fasihi ni chombo muhimu katika kuwasilisha na kuendeleza ajenda ya MME.

Hata hivyo, nyingi zimejikita katika sera, elimu na uchumi, huku nafasi ya fasihi ikipewa kipaumbele kidogo. Pale fasihi inapojadiliwa, mara nyingi huzingatia riwaya au kazi za kimagharibi badala ya tanzu za Kiafrika. Makala hii inaziba pengo hilo kwa kuchunguza jinsi MME yanavyohamasishwa kupitia tamthilia teule za Kiswahili.

### Nadharia ya Utafiti

Kazi hii iliongozwa na nadharia ya Uhistoria Mpya iliyoasisiwa na Stephen Greenblatt (1980) na kuendelezwa na Brizee na Tompkins (2012). Nadharia hii ina mihimili mitatu mikuu. Mhimili wa kwanza ni kuwa masuala ya kifasihi huchunguzwa mintarafu wakati au muhula na mahali. Wa pili ni utunzi wa kazi ya fasihi na jamii ambayo kwayo kazi hiyo imeandikwa ni muhimu na wa tatu ni fasihi inaweza kuelezwa nje ya mtungo wenyewe. Mhimili wa kwanza: masuala ya kifasihi huchunguzwa mintarafu wakati au muhula na mahali na wa pili: utunzi wa kazi ya fasihi na jamii ambayo kwayo kazi hiyo imeandikwa ni muhimu ilifanya kazi hii kufaulu. Kupitia kwa mihimili hii, vipengele vya utunzi wa fasihi vikiwemo fani na maudhui vimetumiwa kubainisha MME katika tamthilia teule kwa mujibu wa muktadha ambamo tamthilia teule zimetungwa.

### MBINU ZA UTAFITI

Utafiti huu ulikuwa wa kithamano na ulitumia muundo wa kiuchambuzi kuchunguza uhamasishaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME) katika tamthilia teule. Data ilikusanywa maktabani kupitia usomaji wa kina wa tamthilia mbili: *Mwinyi na Manyani ya Adili* (Mbogo, 2022) na *Kodi* (Muhando, 2024). Mbinu ya usampulishaji wa kimaksudi ilitumika kuchagua tamthilia hizi mbili. Data ilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji wa kina wa maandishi ya kifasihi. Tamthilia teule zilichunguzwa kwa makini ili kubaini vipengele vinavyohusiana na MME. Katika mchakato huu, data ilitambuliwa na kubainishwa kwa kutumia orodha ya uthibitishaji iliyojumuisha vipengele kama wahusika, mandhari, migogoro, na maudhui yanayohusiana na MME. Orodha hii ilitumika kama mwongozo ili kuhakikisha kuwa vipengele vyote muhimu vinavyohusiana na lengo la utafiti vinatambuliwa kwa usahihi na uthabiti.

Baada ya ukusanyaji, data ilipangwa kwa utaratibu na kisha kuchanganuliwa kwa kutumia mbinu ya uhakiki wa yaliyomo (content analysis). Mbinu hii inahusisha kupanga na kuchambua maandishi kulingana na mada au dhana mahususi (Creswell, 2003; Krippendorff, 2018). Madondoo yaliainishwa kulingana na malengo ya mpango MME, kisha kuchambuliwa ili kubainisha jinsi maudhui, wahusika, migogoro na mazungumzo yanavyoshirikiana katika kuwasilisha uhamasishaji wa MME. Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa njia ya maelezo ya maandishi ya kitaaluma.Masuala ya kimaadili yalipewa kipaumbele katika utafiti huu. Creswell (2003) anasisitiza kuwa mtafiti asidanganye,

asizime au kubadilisha matokeo ya utafiti ili kutosheleza mahitaji yake au ya hadhira. Usahihi wa matokeo umehakikishwa, na marejeleo yote yametolewa ipasavyo. Haki miliki za waandishi zimeheshimiwa. Madondoo yote yaliyotumika yamenukuliwa kwa usahihi bila kuongezwa au kupunguzwa, na kurasa husika zimeonyeshwa.

**MATOKEO YA UTAFITI**

Tamthilia ina uwezo wa kuwasilisha masuala ya kijamii kama uongozi, maadili, dhuluma na maendeleo ya jamii kwa njia ya wazi na yenye mvuto (Mazrui & Mazrui, 1995; Mlama, 1991). Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME) ni ajenda ya kimataifa yenye malengo 17 yanayofungamana na kutegemeana (Barbier & Burgess, 2017; Gosling-Goldsmith, 2018). Makala hii ilichunguza namna baadhi ya Malengo hayo yanavyojitokeza katika tamthilia za *Mwinyi na Manyani ya Adili* (Mbogo, 2022) na *Kodi* (Muhando, 2024).

**Malengo ya Maendeleo Endelevu katika Tamthilia Teule za Kiswahili**

**Lengo 1 (L1): Kutokomeza Umaskini wa Aina Yote Kila Mahali**

Tamthilia ya *Mwinyi na Manyani ya Adili* (2022) inazungumzia uongozi wa kisiasa wa Rais wa pili wa Jamhuri ya Tanzania aliyeitwa Ali Hassan Mwinyi. Utangulizi wa tamthilia hii (uk.iv – vi) unatoa mhutasari wa uongozi wake. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uhistoria Mpya, ambayo ni nadharia iliyotumiwa kufanikisha makala hii, fasihi huchunguzwa mintarafu wakati au muhula na mahali (Davis & Schleifer, 1986).

Kwa kuzingatia matini teule, Nadharia ya Uhistoria Mpya hujikita katika kipindi cha kihistoria ambamo matini husika huwa yametungwa (Brizee &Tomkins (2012). Tamthilia ya *Mwinyi na Manyani ya Adili* inahusu kipindi cha miaka kumi (1985 – 1995) cha uongozi wa kisiasa wa Rais Ali Hassan. Tamthilia hii ina wahusika mbalimbali ambao katika uhalisia waliwahi kuhudumu katika nyadhifa mbalimbali nchini Tanzania. Mifano ya viongozi hawa ambao vilevile ni wahusika katika tamthilia hii ni: Rashid Kawawa, Joseph Warioba na Cleopa Msuya.

Mwandishi wa tamthilia hii, Profesa Emmanuel Mbogo anasuka matukio ya kihalisia katika kipindi cha kihistoria na fasihi. Mhimili wa pili wa Nadharia ya Uhistoria Mpya unaeleza kuwa, utunzi wa kazi ya fasihi na jamii ambayo kwayo kazi hiyo imeandikwa ni muhimu. Nadharia hii husisitiza kuwa, kazi ya kisanaa ni zao la utajiri unaopatikana katika kumbukizi ya visa na matukio muhimu yenye athari kichwani mwa mtunzi, hivyo utunzi wake hubeba historia ya ukweli wa mambo (Davis & Schleifer, 1986; Butler, 1989). Mbogo anatumia matukio halisi ya kihistoria katika uongozi wa Rais Mwinyi kuumba kazi ya fasihi ya *Mwinyi na Manyani ya Adili*.

Nchi ya Tanzania iliongozwa na viongozi waliochaguliwa kupitia mchakato wa kidemokrasia yaani uchaguzi (uk. iv). Baada ya utawala wa Rais wa kwanza Mwalimu Julius Nyerere, wananchi wa Tanzania walimchagua Rais Ali Hassan Mwinyi. Nadharia ya Uhistoria Mpya husisitiza suala la uyakinifu. Kihalisia, Rais Julius Nyerere aliongoza Tanzania kati ya mwaka 1961 hadi 1985 naye Rais Ali Hassan Mwinyi 1985 mpaka 1995. Mwandishi wa tamthilia hii anatumia matukio ya kihistoria nchini Tanzania kuumba upya fasihi mwaka wa 2022.

Umaskini katika tamthilia ya *Mwinyi na Manyani ya Adili* (2022) unachangiwa na Mfumo wa Ujamaa ulioanzishwa na mwanzilishi wa taifa la Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere. Hii ina maana kuwa, aina ya uongozi yaweza kusababisha wananchi kuwa maskini au kuepuka umaskini. Umaskini unatawala nchini Tanzania katika kipindi hiki. Salama akizungumzia hali hii anasema:

> *Wala! Billah Rasul, hujakosea. Raia huko mitaani wananong'ona, wanasema: katika mabadiliko haya ya utawala, labda Mzee Mwinyi anaweza akaturejeshea neema ambayo, imepotea kote nchini…Ukata umechimba makucha yake kila pembe ya nchi hii (uk. 12).*

Maneno ya Salama yanadhihirisha matumaini ambayo raia wa Tanzania walikuwa nayo wakati Rais Mwinyi alikuwa akitwaa uongozi. Kuna mbinu ya tashhisi iliyotumiwa katika dondoo hili ambapo ukata una makucha anaoutumia kuchimba kila pembe ya nchi. Mbinu hii inabainisha namna umaskini ulikuwa umeingia katika kila pembe ya nchi na kuathiri raia kwa njia hasi. Kamusi Sanifu ya Kiswahili, TUKI, 2014 inaeleza umaskini kama hali ya kukosa mali. Ukosefu katika tamthilia ya *Mwinyi na Manyani ya Adili* unatokana na Mfumo wa Ujamaa ambao ulifanya

baadhi ya bidhaa kama vile kolgeti na sabuni ya kuogea kama *Lux* kupigwa marufuku. Jambo la kushangaza ni kwamba hata Ikulu, umaskini umetawala. Siti, mkewe Mwinyi anasema:

> *Kabisa! Ulitima na ukata umepiga hodi na kutamalaki hata Ikulu! Ee! i-ku-lu! First lady anajikuta hana hata sabuni ya kuogea! Na ili kuondoa harufu kinywani, inanibidi nisukutue kwa maji ya karafuu! (uk.2)*

Zamda ambaye ni mtumishi wa Siti na Mwinyi anakiri kumuona Siti akiogea sabuni ya kufulia nguo kwa kuwa amekosa sabuni ya kuogea (uk. 2). Hali hii ya umaskini kutawala mpaka Ikuluni inachora taswira ya utamaushi nchini.

Msuya ambaye alikuwa mmoja wa viongozi katika enzi ya rais mtangulizi Mwalimu Nyerere akizungumzia hali ya umaskini anasema:
*"Watu! Raia kote nchini wanateseka. Umasikini ulioikumba nchi yetu, haujawahi kutokea tangu tupate uhuru. Uchumi wa nchi yetu, ndugu Rais, ulikuwa ICU! Karibu kukata roho! ." (uk.54-55)*

Inabainika kupitia maneno haya ya Msuya kuwa kiwango cha umaskini kilichoshuhudiwa wakati wa uongozi wa Rais Nyerere hakijawahi shuhudiwa katika historia ya nchi ya Tanzania. Uchumi ulikuwa umedorora sana.

Henzirani ambayo inatumiwa na Baraza kuadhibu manyani wawili kikatili katika tamthilia ya *Mwinyi na Manyani ya Adili* ni jazanda ya umaskini ambao uliwatesa wananchi. Kiongozi Mwinyi akiwahutubia wananchi anawaeleza:

> *Unakutana na maduka yaliyojaa mende na panya badala ya bidhaa mbalimbali za kumkimu binadamu. Umasikini! Umasikini! Umasikini!! Ufukara na uchochele ndugu zangu ni mjeledi unaoumiza sana. Ni henzirani yenye uwezo mkubwa wa kudhalilisha utu na heshima ya binadamu kupitia maelezo. (uk. 41)*

Hotuba hii ya rais inaonyesha namna umaskini ulivyokuwa donda ndugu nchini. Aidha, inadhihirisha athari hasi ya umaskini ya kufanya binadamu akose utu na heshima. Kawawa ambaye alikuwa waziri mkuu katika utawala wa Rais Nyerere anasema:
*"Watu wamedhalilishwa na ufukara kiasi cha kutosha. Watu wametembea uchi kiasi cha kutosha. (uk.57)."*

Kupitia uradidi wa maneno: kiasi cha kutosha kiwango cha juu cha umaskini uliotawala kote nchini kinasisitizwa. Umaskini huu unabainika kupitia ukosefu wa vitu vya kimsingi kama sabuni, dawa ya meno na mavazi. Akizungumzia mavazi Rais Mwinyi anasema kuwa wananchi hawana nguo. Anakiri kuwaona wengine mikoani wakitembea uchi (uk.24).

Baada ya kuutwaa uongozi, Rais Mwinyi anachukua hatua ya kupambana na hali hii ya umaskini uliokithiri kipeo kila pembe ya nchi. Njoroge (2014) kupitia utafiti wake anadai kuwa viongozi ni vichochezi na visababishi vya maendeleo. Rais Mwinyi anachochea na kusababisha maendeleo nchini kupitia mikakati mbalimbali kama vile wa kutupilia mbali Mfumo wa Ujamaa na kuruhusu mfumo wa sokohuria. Kupitia mabadiliko ya kisheria yaliyowahusisha wananchi na bunge, anaruhusu wananchi kujihusisha katika shughuli za kujiinua kiuchumi. Mojawapo wa shughuli hii ni biashara. Anawaruhusu raia kufanya biashara ndani mwa na nje ya nchi. Mikakati hii ya kiongozi Mwinyi zinapunguza kiwango cha umaskini nchini.
Mtei anasema kuwa:

> *…ghafla neema imeanza kujitokeza kote nchini (uk.56). Wananchi wanafurahia kuimarika kwa maisha. Mfano ni Abu na Zahara wanaokaa mtaa wa Kariakoo. Abu na Zahari wanazungumzia mabadiliko ya Rais Mwinyi yaliyoboresha maisha. (uk. 63, 65)*

Inabainika kuwa, uongozi wa Rais Mwinyi unaweka mikakati ambayo inachangia kupunguza kiwango cha umaskini cha raia wa Tanzania. Mikakati hii inaendeleza uafikiaji wa L1.

**L2: Kutokomeza Njaa, Kuwa na Uhakika wa Chakula, Lishe Bora na Kukuza Kilimo**

Kwa mujibu wa tamthilia ya *Mwinyi na Manyani ya Adili*, kiongozi Mwinyi anachukua hatamu za uongozi katika kipindi kigumu katika historia ya taifa la Tanzania. Njaa ilikuwa imetawala kote na kuwaathiri wananchi kila pembe ya nchi. Mwinyi anakiri hali hii anaposema: Watu wanajaa (uk. 23). Hali hii ya njaa inasababishwa na Mfumo wa Ujamaa ambao uliendelezwa na Rais mtangulizi. Akiwahutubia wananchi, Mwinyi anawaambia:

> *Lakini baada ya miongo hiyo mitatu, imedhihirika dhahiri shahiri kuwa changamoto na matatizo yamekuwa mengi zaidi. Na labda hata yamekuwa magumu zaidi. Hata yamekuwa machungu zaidi kiasi kwamba kila kona ukipita hapa nchini unakabiliana na nyuso zenye huzuni, badala ya furaha; nyuso zenye hofu badala ya matumaini; Nyuso zenye njaa badala ya shibe... (uk. 40-41)*

Inabainika kupitia hotuba hii kuwa, njaa imetamalaki kote nchini na imesababisha huzuni, hofu na ukosefu wa matumaini miongoni mwa wananchi. Rashid Kawawa, aliyekuwa waziri mkuu katika utawala wa Rais Julius Nyerere anasema:
*"Njia nzima hakuna chakula. Kuna njaa na ufukara...." (uk.57)*

Njia anayoirejelea kiongozi Kawawa ni jazanda ya enzi ya utawala wa Rais Nyerere. Katika kipindi hiki cha uongozi, njaa ilikuwa jambo la kawaida nchini Tanzania. Awali, Arafat na Anifa walikuwa wanajeshi (uk.2). Kwa sababu ya matendo yao yaliyopinga Mfumo wa Ujamaa, wanapigwa na maafisa wa polisi hadi wanazirai na kufa. Wanatupwa gerezani na kusafirishwa visiwa vya Mafia ambapo waligeuka kuwa nyani (uk. 100). Baada ya kurudishiwa ubinadamu wao. Arafat anakumbuka siku walipopigwa na kuzirai. Anasema:

> *Nakumbuka siku maafa haya yalipotokea, tulikuwa tumeenda mwendo mrefu tukisaka chochote ili tutie mkono kinywani...lakini baada ya mwendo mrefu, hamadi! Tukajikuta tumetokezea kunako shamba la miwa na ndizi. Tukatabasamu, Tukasemezana: "Hatutaiba kisicho chetu. Ni dhambi kwa Mwenyezi Mungu. Basi na tuokote na tule makumbo haya yalidondoka chini!" Haya! Tukaokoteza! Tukaokoteza, tukala, tukala (uk. 99).*

Motifu ya safari katika maneno haya ya Arafat ni jazanda ya enzi ya utawala wa Rais Nyerere. Katika enzi hii, wananchi wa Tanzania wanakabiliwa na tatizo la njaa linalowafanya wasake kitu chochote ili watie kinywani. Wale wanaobahatika kupata mabaki yaliyoachwa na viongozi wanakula kwa pupa ili kuponya njaa.

Kupitia mbinu rejeshi anayotumia mwandishi Emmanuel Mbogo, Mtei anamkumbusha Rais Mwinyi pamoja na viongozi wengine namna alivyomwambia Rais Nyerere kuwa tatizo la njaa nchini lilisababishwa na Mfumo wa Ujamaa. Anasema:

> *Nilimwambia: Ndugu Rais, marimba na kamsa za ujamaa na kujitegemea, zimeshindwa kuwapa watu wako walau tonge la mkono kinywani. Wanaume wenye wake na watoto, wengi wao wamevunja amri ya Paulo inayosema: Mzazi yeyote anayeshindwa kumkimu mke na watoto wake ni kafiri kuliko ibilisi! (uk. 55 – 56).*

Kutokana na maneno haya ya Mtei, tunabaini kuwa, tatizo la njaa limechangiwa pakubwa na hali ngumu ya kiuchumi ambayo ni zao la Mfumo wa Ujamaa. Kwa sababu ya hali hii, wazazi hawawezi kukimu mahitaji ya familia zao. Kwa sababu ya njaa iliyokithiri nchini, wananchi wanalazimika kula unga wa manjano uitwao dobesi (uk. 65). Wanapokula ugali uliopikiwa na unga huu wanakuwa na tatizo la kupitisha choo wakiwa msalani (uk. 66).

Alipotwaa uongozi, Rais Mwinyi anakabiliwa na tatizo la njaa. Anafutilia mbali Mfumo wa Ujamaa. Anasema kuwa watu hawawezi kula itikadi (Itikadi ya ujamaa) (uk.36). Anaruhusu Mfumo wa Sokohuria (uk.40). Matokeo ya hatua hii ya kijasiri ya kiongozi Mwinyi ni kutokomezwa kwa njaa. Siti akizungumzia hali iliyoimarika nchini anasema:
*"Jangwa kaligeuza pepo. Njaa kaigeuza shibe. Nyuso zenye huzuni, kazivika tabasamu, bashasha na vicheko. Upo hapo! " (uk. 77)*

Njaa inabadilika na kuwa shibe. Badala ya kuhuzunika, wananchi wanapata furaha. Zahara anazungumzia kuimarishwa kwa hali kupitia uongozi wa Mwinyi. Anamwambia Abu:
*"Hapa mjini kila mtu ana pesa. Katika familia, kila mtu anakula anashiba. Alhamdulillah rabil alamin!" (uk.65).*

Dondoo hili linabainisha juhudi za kiongozi Mwinyi kuafikia L1 na L2. Kwa mujibu wa Njoroge (2014), viongozi husababisha na kuchochea maendeleo. Rais Mwinyi anachochea na kusababisha maendeleo nchini Tanzania ambayo yanapunguza njaa na umaskini.

**L5: Kufikia Usawa wa Kijinsia na Kuwawezesha Wanawake na Wasichana Wote**

Kwa kurejelea tamthilia ya *Kodi* (2024), wanawake katika nchi rejelewa walikuwa wakikandamizwa kwa sababu ya jinsia yao. Mosi ni kuwa, ubakaji ulikuwa ukiendelezwa nchini (uk.38- 39). Aidha, kunao wanawake wanaopitia dhuluma za kifamilia katika nchi hiyo. Wanawake hawa wanawakilishwa na mama ambaye anapigwa na mumewe. Mama anasema:

*"Kanipiga. Kanipiga tena. Leo sikubali." (uk. 39)*

Kwa mujibu wa Uhistoria Mpya, utunzi wa kazi ya fasihi ni muhimu. Kwa kurejelea usemi huu wa Mama, takriri ya neno kanipiga na matumizi ya neno tena yanaashiria kuwa si mara ya kwanza mumewe mama huyu kumpiga. Amempiga mara kadhaa jambo linalomfanya mama kukimbilia kuripoti katika kituo cha polisi ili apate haki kwa kuwa amechoshwa na mapigo ya mara kwa mara. Huku bado akilia, mama anasema: Kanipiga, kanipiga sana! Baada ya kusema hivi anaendelea kulia kwa nguvu. Kwa kurejelea dondoo hili, maneno kanipiga sana na tendo la kulia linaonyesha mapigo yalikuwa ya kinyama. Mama anaendelea kusema:

*"Na ufungwe! Leo sikubali. Nimechoka mateso!" (uk.39)*

Anaposema kuwa amechoka mateso, anaanza kulia. Tendo hili linaonyesha kuwa mama amepitia mateso katika ndoa. Usakaji wa haki wa mama huyu unakumbwa na changamoto kwani sauti katika jamii inamshutumu kwa tendo la ujasiri alilochukua kutafuta haki katika kituo cha polisi. Sauti ya wanajamii inamwambia:

*"Ukimshtaki polisi ujue mumeo ndio atafungwa." (uk.39)*

*"Wewe utamfungaje mumeo?" (uk. 39)*

Kinaya ni kuwa badala ya polisi kumsaidia, wanamweka ndani. Mama anashangazwa kwa hili. Anateta dhidi ya uonevu huu:

"Unaniweka ndani mie nimekosa nini? Mie namshtaki mume wangu halafu unataka kuniweka ndani mie! Kosa langu nini?" (uk.40)

Tendo la mama kuteta dhidi ya mapigo linaashiria wanawake waliochoka na dhuluma za ndoa na wanajitokeza kupinga dhuluma hizi. Wanatetea usawa wa kijinsia katika taasisi ya ndoa. Kiongozi anayewajibika anafaa kuchukua hatua zinazolenga kukomesha dhuluma dhidi ya wanawake na kuwawezesha wanawake kupitia miradi ya kuinua hali zao za kiuchumi, kielimu na kisiasa. Hakuna kiongozi anayetekeleza jambo hili katika nchi ya Kodi. Kinyume na matarajio haya, askari katika *Kodi* wanaendeleza dhuluma dhidi ya wanawake.

Kando na kupigwa na waume zao, jinsia ya kike inaachiwa majukumu ya kifamilia na waume zao. Wanaume wanakosa kuwajibikia familia zao. Mariam anamwambia Shangwe:

*"Mie hata sijui kama shuleni kwenyewe nitarudi tena. Najua baba yangu hatalipa ada kabisa." (uk.29).*

Mariam alikwisha kujua kwamba baba yake hangelipa karo ya shule. Aidha, Mama Shangwe anajikuta kugharamia mahitaji ya nyumbani pekee yake bila usaidizi kutoka kwa mumewe (uk.21). Hali inapozidi anateta dhidi ya unyanyasaji huu. Anamwambia mumewe kuwa haondoki nyumbani bila kuacha hela za matumizi (uk.23).

**L8: Kazi zenye Staha na Ukuaji Kwa Wote**

Suala la kazi limeangaziwa katika tamthilia ya *Mwinyi na Manyani ya Adili.* Suala hili limegawika katika vipindi viwili: Kipindi cha utawala wa Rais Nyerere (kipindi kabla ya utawala wa Rais Mwinyi) na kipindi cha utawala wa Rais Mwinyi. Wakati wa utawala wa Nyerere (Mfumo wa Ujamaa), watu walifanya kazi pamoja. Mathalani walilima mashamba pamoja. Upamoja huu ulikuza amani na umoja (uk.52-53). Hata hivyo, Mfumo wa Ujamaa uliendeleza uzembe na hatimaye kusababisha umaskini. Hivyo basi, wachache waliojibidiisha kazini hawakufurahia kazi yao. Isitoshe, uchumi ulikuwa umezorota. Umaskini ukaenea kote.

Awali, Anifa na Arafat wanafanya kazi ya ukapteni jeshini. Kwa sababu ya hali mbaya ya umaskini iliyokuwa imetawala nchini, wanaunda chama na kuandika kitabu- vyote vilivyopinga ujamaa. Kikosi maalum cha polisi kinawapiga mijeledi ambayo inawafanya wazirai na kufa. Wafapo, wanageuka manyani. Badala ya kazi yao ya ukapteni kuleta furaha kwao inawaletea mateso na maafa (uk.99-100). Baraza ni mfanyakazi anayewatunza manyani wawili. Ionekanavyo, Baraza anafanya kazi ila kazi aifanyayo haina heshima. Inabidi awapige nyani kutumia henzirani (uk.18).

Aidha, anakula pamoja na nyani (uk.34). Baraza ni kiwakilishi cha wafanyakazi ambao walichapwa kwa hali ngumu ya maisha wakati wa utawala wa Rais Nyerere na kulazimika kufanya kazi ambazo hazikuwa na heshima. Kipindi cha pili ni kipindi cha utawala wa Mwinyi. Katika kipindi hiki, wafanyakazi wanaonekana kufurahia kazi wazifanyazo kwani zina tija. Abu ambaye ni muuza magazeti na Zahara ambaye ni muuza nguo za wanawake, vipodozi na nguo za wanaume wanafurahia kazi zao. Wanaamka asubuhi mapema kuelekea sokoni Kariakoo. Abu anamwambia Zahara:

*"Sasa nchi imekuwa tamu! Maisha matamu kama asali." (uk. 63)*

Zahara vilevile anasema kuwa katika Mfumo wa Sokohuria kila familia ina shibe; kila mtu ana pesa (uk.65). Aidha, Halima na Mwanaisha wanafanya kazi ya staha. Wanafanya kazi ya kutembeza bidhaa hasa mapambo na mavazi ya kuwarembesha wanawake. Wanazitoa bidhaa hizi Dubai na kuzileta nchini Tanzania. Wanaifanya biashara hii kwa furaha. Halima anamwambia Siti:

> *Nyumbani mama! Tunaenda mji wote tukiwasaka wateja wetu. Usione hivi. Mabegi haya yatakuwa tupu ifikapo jioni. Inaitwa Ngekewa ya Rukhsa! Rukhsa! Rukhsa! Pesa na utajiri ndiyo sabuni na marashi ya moyo. Mama Rukhsa! (uk.80).*

Maneno haya ya Halima yanabainisha watu wenye furaha, wanaofurahia kazi yao ambayo inawapa staha katika jamii na kuwafanya wakue kiuchumi. Inadhihirika kupitia muktadha huu kuwa viongozi wana nafasi muhimu katika kubuni nafasi za ajira zenye staha kwa ajili ya wananchi. Rais Mwinyi anafanya maamuzi ya kuwaruhusu wananchi kujihusisha katika biashara ndani na nje ya nchi ya Tanzania. Alivyoshadidia Njoroge (2014), viongozi ni visababishi na vichochezi vya mabadiliko. Kiongozi Mwinyi anachochea na kusababisha mabadiliko ya mfumo wa kiuchumi; mabadiliko ambayo yanaboresha hali ya kiuchumi ya wananchi. Onyesho la saba linapoanza tunawaona mafundi wawili wakiwa ukumbini mwa Ikulu. Mafundi hawa wanafunga king'amuzi cha runinga. Wanaonekana kufurahia kazi yao (uk.74- 75).

**L11: Kuweka Miji na Makazi ya Binadamu Kuwa Jumuishi, Salama, Imara na Endelevu**

Kwa mujibu wa tamthilia ya *Kodi*, kunalo tatizo la miji kuwa michafu. Viongozi wa nchi wana jukumu la kuhakikisha usafi wa miji. Miji ikiwa michafu, kutatokea magonjwa yanayoweza kuleta maafa. Inabainika kupitia tamthilia hii kuwa, viongozi walikosa kuweka mikakati ya kudumisha usafi wa miji. Hali hii ilisababisha aibu. Konje anasema:

*"Jamani mji wetu ni mchafu. Nani anabisha? Aibu! Wageni wa heshima wanakuja. Mji ni mchafu kwelikweli." (uk. 53)*

Uradidi wa neno mchafu katika muktadha huu unasisitiza aibu iliyokuwa imesababishwa na uchafu uliokuwa umekithiri mjini. Ili kusuluhisha tatizo hili, tenda inatangazwa. Kikundi cha kina mama kinajitokeza kufanya kazi hii. Kundi hili linasema kuwa litasaidiana na watoto wao ambao ni vijana. Mtu 3 anasema:

"Kazi hii haitatushinda. Tutasafisha barabara, tutafagia uwanja, vyoo tutasugua kabisa, mji wote tutasafisha, kote!" (uk.54)

Usemi huu unabainisha kuwa, majivu, makaa, uchafu wa mafuta kutoka mikahawani, taka kutoka kwa vibanda vya kibiashara; moshi kutoka kwa wachoma mahindi na makoroboi na maskrepa ni baadhi ya vitu vinavyouchafua mji (uk. 54). Inajitokeza kuwa, usafi wa mji utaondoa aibu, utavutia wageni, utahakikisha magari yanapita bila tatizo, utatokomeza nzi na mijusi (uk.54-55). Mji safi utakuwa fahari ya wananchi hivyo kuendeleza uafikiaji wa L11:

> Mji kuwa safi fahari yetu…
> Nitausafisha mji ukageuke kioo
> Mainzi wasisogee mijusi watokomee (uk. 55).

**L16: Kuendeleza Jamii Jumuishi na Yenye Amani kwa Ajili ya Maendeleo Endelevu, Kutoa Haki kwa Wote na Kujenga Taasisi Imara zenye Kuwajibika katika Nyanja Zote**

Kwa kurejelea tamthilia ya *Kodi* (2024), haki za walemavu zimeangaziwa. Kuangaziwa huku kunalenga kuondoa unyanyapaa, kuendeleza haki na kuhakikisha kuwa jamii ni jumusihi na yenye usawa. Kuangaziwa huku kunafanyika kupitia kwa taasisi ya elimu. Mariamu anasema:

"Wee, mwalimu kasema tusiwaite 'viziwi'. Wenyewe hawataki kuitwa hivyo. Wanaitwa 'wasiosikia', siyo 'viziwi'." (uk.5)

Kwa mujibu wa muktadha wa dondoo hili, Mwalimu, ambaye ni kiwakilishi cha kiongozi katika sekta ya elimu anawafunza wanafunzi wakiwemo Mariamu na Shangwe lugha watakayoitumia kuepuka unyanyapaa dhidi ya walemavu. Jambo hili ni muhimu katika kujenga jamii jumuishi ambayo inalinda na kuheshimu haki za walemavu.

Mama Shangwe anaponyimwa fursa ya kujieleza katika hafla ya kutafuta watu watakaopewa tenda, anaitetea haki hii. Anasema: "Na mimi lazima nijieleze..." (uk. 58)

Aaah! Na mimi nataka kujieleza. Mapishi najua sana mimi. Na mimi tenda naitaka. Naona yanaletwa mambo ya upendo hapa." (uk. 58). Inapombainikia kuwa amepuuzwa na kwamba tenda imetolewa kwa upendeleo, anatetea haki yake ya kujua nani aliyeteuliwa. Konje, Mwidiki 1 na Mwidiki 2 wanampuuza Mama Shangwe. Hata hivyo, hakati tamaa. Anaapa kwenda mbele: Anasema:
*"Lakini mimi sioni usawa wowote hapa. Mimi nitakwenda mbele nakwambieni; maana hii ni haki yangu ya msingi." (uk.59)*

Mariam na Shangwe wanatetea haki yao ya kucheza ngoma siku ya watoto duniani. Licha ya ngoma yao kupigwa marufuku Shangwe anaapa kucheza ngoma hii. Anasema:
*"Ngoma lazima nitacheza. Na sisi tuna haki ni kama watoto wengine." (uk.72)*

Mwandishi Penina Muhando anatueleza:
Linaingia kundi la vijana kwa maandamano, wamebeba mabango yaliyoandikwa: *"Tunataka haki zetu"; "Na sisi tunataka kodi zetu," "Kodi ni haki."* Wanaimba (uk.128).

Maelezo haya ya mwandishi yanachora taswira ya watu walioamua kutetea haki zao kupitia maandamano. Maandamano haya yanalenga kushinikiza serikali ya nchi hii kuwajibikia kuwapa haki kama vile za kumiliki mashamba, kuajiriwa, kupewa tenda na kutonyanyaswa kiuchumi kupitia ulipaji kodi kupindukia. Hali hii inaendeleza uafikiaji wa L16.

Maandamano ni njia mojawapo zinazotumiwa kushinikiza mabadiliko katika jamii. Mathalani, nchini Kenya, mwaka wa 2024 ulishuhudia maandamano ya kupinga Muswada wa Fedha. Maandamano haya yaliongozwa na vijana. Kwa mujibu Jahazi (2025) vijana hawa walitumia mikakati mipya ambayo haijazoeleka kama vile mitandao ya kijamii: *Tiktok*, *X* na *Watsup* pamoja na vyombo vya habari. Maandamano haya yalichochea mjadala kuhusu nguvu halisi za teknolojia na maandamano katika kuleta mabadiliko ya kisiasa na maendeleo (Jahazi, 2025).

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

**Hitimisho:** Kazi hii imewasilisha matokeo na mjadala kuhusu MME yanayobainika katika tamthilia za Mwinyi *na Manyani ya Adili* (Mbogo, 2022) *na Kodi* (Muhando, 2024). Kazi hii imebaini kuwa tamthilia za Mwinyi *na Manyani ya Adili* (Mbogo, 2022) *na Kodi* (Muhando, 2024) ni jukwaa ambalo limetumiwa na waandishi kuhamasisha kuhusu malengo mbalimbali ya mpango wa MME hasa L1 (kutokomeza umaskini), L2 (kutokomeza njaa), L5 (usawa wa kijinsia), L8 (ajira na uchumi), L11 (miji na makazi endelevu) na L16 (amani, haki na taasisi imara). Imedhihirika kuwa, masuala ya usawa, jamii jumuishi na miji na makazi ya binadamu yanajitokeza kupitia migogoro ya wahusika na hali zao za maisha, huku njaa, umaskini na kazi yakibainika kupitia maamuzi na matendo ya viongozi katika tamthilia hizo. Utafiti huu umetambua kuwa, malengo mengine kama L3 (afya bora), L4 (elimu bora), L6 (maji safi na usafi wa mazingira), L7 (nishati safi), L9 (viwanda na ubunifu), L10 (kupunguza ukosefu wa usawa), L12 (matumizi endelevu), L13 (hatua dhidi ya mabadiliko ya tabianchi), L14 (maisha chini ya maji) na L15 (maisha ya nchi kavu) hayajaangaziwa kwa kina au yamepuuzwa kabisa kwa mujibu wa tamthilia rejelewa.

**Mapendekezo:** Makala hii inapendekeza kuwa waandishi wa tamthilia za Kiswahili wapanue wigo wa maudhui kwa kujumuisha kimaksudi Malengo yaliyopuuzwa, hasa L3, L4 na L6, ili kuimarisha mchango wa fasihi katika uhamasishaji mpana wa MME**.** Aidha, watafiti wa baadaye, wachunguze MME yanavyojitokeza na kuafikiwa katika tanzu zinginezo za fasihi kando na tamthilia ambayo imerejelewa na utafiti huu. Mathalani wanaweza kurejelea riwaya, ushairi au hadithi fupi na fasihi simulizi.

**MAREJELEO**

Barbier, E. B., & Burgess, J. C. (2017). The Sustainable Development Goals and the systems approach to sustainability economics. *Economics, 11*(1), 1–22. https://doi.org/10.5018/economics-ejournal.ja.2017-28
Bebbington, J., Unerman, J., & O'Dwyer, B. (2014). *Sustainability accounting and accountability*. Routledge.
Brizee, A., & Tompkins, J. C. (2012). New historicism, cultural studies (1980s–present). Purdue University.
Butler, M. (1989). *Rethinking historicism: Critical readings in romantic history*. Oxford University Press.
Browne, E., & Millington, K. A. (2015). *Social development and human development: Topic guide*. GSDRC, University of Birmingham / HEART.
Creswell, J. W. (2003). *Research design: Qualitative, quantitative, and mixed methods approaches* (2nd ed.). Sage Publications.
Davis, R. C., & Schleifer, R. (Eds.). (1986). *Contemporary literary and cultural criticism*. Longman.
Edler, K. L., & Park, J. (2021). Culture and the Sustainable Development Goals: An outlook of future opportunities. *United Nations University Working Paper*. United Nations University.
Gosling Goldsmith, J. G. (2018). *Sustainable Development Goals and uncertainty visualization* (Unpublished master's thesis). University of Twente.
Greenblatt, S. (1980). *Renaissance self-fashioning: From More to Shakespeare*. University of Chicago Press.
Jahazi. (2025). Arts, digital technology & the Gen Z protests in Kenya. *Twaweza Communications*.
Krippendorff, K. (2018). *Content analysis: An introduction to its methodology* (4th ed.). Sage Publications.
Magendane, K., & Kapazoglou, M. (2021). Approaches to study SDG interactions: Literature review of relevant frameworks. University of Amsterdam.
Mazrui, A. M., & Mazrui, A. A. (1995). *Swahili state and society: The political economy of an African language*. East African Educational Publishers.
Mazza, P. I. (2021). Concepts of sustainable development: A literature review and a systematic framework for connecting the role of education with the Sustainable Development Goals (SDGs). *International Journal of Humanities Social Sciences and Education, 8*(8), 106–112. https://doi.org/10.20431/2349-0381.0808009
Mbogo, E. (2022). *Mwinyi na Manyani ya Adili*. Africa Proper Education Network.
Mensah, J. (2019). Sustainable development: Meaning, history, principles, pillars, and implications for human action: Literature review. *Cogent Social Sciences,* 5(1), 1–37. https://doi.org/10.1080/23311886.2019.1653531
Mlama, P. M. (1991). *Culture and development: The popular theatre approach in Africa*. UNESCO.
Muhando, P. (2024). *Kodi*. Mbiu Press.
Musindalo, M. A. (2020). *Taswira ya haki za watoto katika riwaya teule za Kiswahili za milenia mpya* (Unpublished master's thesis, Maseno University, Kenya).
UNESCO. (2024). *Culture and Sustainable Development Goals*. UNESCO Publishing.
United Nations. (2022). *Sustainable Development Goals report 2022*. https://unstats.un.org/sdgs/report/2022/
United Nations. (2023). *Sustainable Development Goals report 2023*. https://unstats.un.org/sdgs/report/2023/
United Nations. (2024). *Sustainable Development Goals report 2024*. https://unstats.un.org/sdgs/report/2024/